

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA



**TANGAZO LA MKOPO WA HAZINA KWA WATUMISHI WA UMMA  
TAREHE 19.12.2024**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma inapenda kuwajulisha Watumishi wote kuwa imepokea Mgao wa Fedha za Mikopo kwa Watumishi kutoka HAZINA kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mkopo huu unatolewa kwa ajili ya Kununua Magari/Pikipiki, Samani na matengenezo ya Magari na Pikipiki kama ilivyofafanuliwa katika Waraka wa Watumishi Na.3 wa mwaka 2012.

Mnatakiwa kuwasilisha maombi yenu ya mkopo kupitia mfumo wa **HAZINA PORTAL** kwa kutumia link ya <https://als.muse.go.tz> kabla au ifikapo **26 Desemba, 2024**.

Aidha mnatakiwa kufahamu kuwa Mtumishi anayetakiwa kukopa lazima awe anakopesheka (Lazima abaki na theluthi (1/3) ya Mshahara wake), asiwe na mkopo mwingine kutoka HAZINA, amethibitishwa kazini na asiwe na mashtaka ya kinidhamu.

Mnashuriwa kuwasilisha maombi yenu ndani ya muda ulipangwa ili kurahisisha kufanyika kwa mchakato wa zoezi hili kwa wakati, mwombaji atakayeomba nje ya muda huo maombi yake hayatoshughulikiwa.

Imetolewa na.

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Jabil Z. Timbako".

Jabil Z. Timbako

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA KIGOMA**

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
KIGOMA**